LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

# Tamko Kukemea Uvamizi wa Uhuru wa Vyombo vya Habari

Jumanne Machi 21, 2017
Dar es Salaam, Tanzania.

**Ndugu Wanahabari,**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za Mkuu wa Mkoa wa Dare es Salaam, Bwana Paul Makonda kuvamia kituo cha Clouds Televisheni kwa kile kinachodaiwa kuwa ni kushindwa kwa juhudi zake za kushinikiza kurushwa kwa taarifa katika kipindi cha The Weekend Chat Show. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimechelea kuamini taarifa hii ambayo ilisambaa mitandaoni tangu usiku wa kuamkia Jumamosi Machi 18, 2017 kwa kile inachoona kuwa ni ukiukwaji mkubwa sana wa misingi ya uhuru wa habari sambamba na misingi ya utawala wa sheria.

Tunatambua uwepo wa sheria kandamizi kwa vyombo vya habari ambazo hupelekea viongozi kutishia na hata kufungia vyombo vya habari lakini kitendo cha kuvamia chombo cha habari ni kigeni na cha kuogofya kwa watanzania.

**Ndugu Wanahabari,**
Vyombo vya habari vinapaswa kulindwa na kupewa ulinzi wa kutosha na si kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote kwa manufaa binafsi yasiyo na tija kwa taifa. Vyombo vya habari vipo kwa mujibu wa sheria na vinaongozwa na sheria kadhaa ikiwemo Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 na hivyo kwa namna yoyote ile vinapaswa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria na si kwa kuingiliwa na mtu binafsi au mamlaka. Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari imeeleza wazi mamlaka ambazo zina weza kuviwajibisha vyombo vya habari pale ambapo vitaonekana vinaelekea au vinatoa habari za uchochezi kama kifungu cha 49(1) na 50(1) na pia mamlaka zenye uwezo wa kutwaa mali yoyote ya chombo cha habari pale kinapokiuka utaratibu halali kwa mujibu wa Sheria kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 56 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari.

**Ndugu Wanahabari,**
Pale inapotokea watu binafsi au mamlaka kutumia nafasi walizo nazo kutaka kushinikiza habari fulani kutolewa na vyombo vya habari kwa maslahi binafsi huko ni kukiuka misingi ya sheria. Na pale ambapo jambo hilo linafanywa na mtu mwenye mamlaka ya kuhakikisha utekelezwaji wa sheria na ulinzi wa amani katika mkoa kwa Mujibu wa sheria ya Tawala za Mikoa kifungu 5

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson, Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Dr. Ringo W. Tenga (Adv) - Member, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member, Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member

kifungu kidogo cha 1 ni jambo la kihuni na la kupingwa kwa nguvu katika taifa linalofuata misingi ya Haki na utawala wa sheria.

**Ndugu Wanahabari**,
Matumizi mabaya ya Vyombo ya Dola katika kudidimiza uhuru wa Vyombo vya habari ni jambo ambalo linapaswa kukemewa vikali kwani jambo hilo linavunja misingi hiyo iliyowekwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 ibara ya 18. Uvunjaji huu wa sheria sio wa kufumbiwa macho hata mara moja.

Aidha jitihada zinazofanywa na Serikali ya awamu ya Tano ya kuhamasisha uwajibikaji ikiwa na kauli mbiu ya HAPA KAZI TU! inatakiwa kuwa chachu ya kulinda misingi ya sheria na taratibu husika na isitumike kama kichaka cha kuvunja sheria na taratibu nyingine zilizopo kwa mujibu wa katiba ya nchi.

Kulingana na hali ilivyo sasa, Kituo Cha Sheria na haki za Binadamu Kitaendelea kukemea vitendo kama hivyo ambavyo vinaidhalilisha serikali kitaifa na Kimataifa kama nchi inayo jipambanua kuwa kisiwa cha amani na mlinzi wa haki za hinadamu na misingi ya utawa bora wenye kulinda Demokrasia.

**Ndugu Wanahabari;**
Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu tunatoa wito kwa Serikali na wadau wengine kuzingatia yafuatayo;

1. Serikali imchukulie hatua za kinidhamu na kijinai Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Bwana Paul Makonda mara moja, kwa kitendo alichokifanya ambacho ni kosa la jinai chini ya kanuni za Makosa ya Adhabu ya mwaka 2002.

2. Viongozi kuacha mara moja matumizi ya vyombo vya dola kwa manufaa binafsi kama ilivyotumika kuvamia kituo cha Television cha Clouds.

3. Serikali kupitia Wizara ya Habari kurejea mapendekezo ya wadau juu ya sheria kandamizi kwa uhuru wa habari ili kutoa ulinzi kwa vyombo vya habari na wanahabari, badala ya kuibuka katika tukio moja moja.

4. Vyombo vya habari kuungana kutetea maslahi ya uhuru wa habari na kuacha kujiendesha kwa maslahi binafsi huku vikiacha weledi wa vyombo hivyo ukizidi kudidimia.

5. Watanzania kwa ujumla wetu tuendelee kukemea tabia kama hizi na kuita uwajibikaji popote pale tulipo.

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson, Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Dr. Ringo W. Tenga (Adv) - Member, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member, Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamau tunaamini serikali kupitia viongozi wake wanafanya kazi kubwa katika kupambana na umasikini , kuboresha elimu, kupinga madawa ya kulevya,

kupambana na Rushwa na kadhalika laniki tunazidi kusisitiza sana viongozi waheshimu misingi ya Utawala Bora na haki za binadamu ili kuifikia jamii yenye Haki na Usawa.

**Imetolewa na:**

**Dr. Helen Kijo Bisimba'**
**Mkurugenzi Mtendaji**

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Athanasia Soka(Adv) - Vice Chairperson, Dr. Helen Kijo-Bisimba - Secretary, Dr. Ringo W. Tenga (Adv) - Member, Mr. Francis Stolla (Adv) - Member, Ms. Emeline Mboya - Member, Ms. Pili Mtambalike - Member Mr. Thaddeo W. Mashera - Member